TAARIFA YA WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB) KUHUSU UENDESHAJI NA UTOAJI WA HUDUMA ZA TIBA KATIKA HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA, 2 JULAI, 2018

Ndugu Wanahabari,

Mnamo Novemba 25, 2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa akizindua Hospitali ya Taaluma na Tiba (MAMC) ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) pia aliagiza kuwa Hospitali za Rufaa za Mikoa zihamishiwe kwenye usimamizi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (WAMJW) kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI. Katika maagizo yake, Mheshimiwa Rais alikusudia kuimarisha usimamizi wa utoaji huduma katika Hospitali hizi, na pia kuhakikisha kuna mgawanyo wenye uwiano mzuri wa Madaktari katika hospitali zote nchini ili, kuepuka uwepo wa Madaktari wengi kuwa katika sehemu moja huku maeneo mengine yakiwa na uhaba mkubwa.

Ndugu Wanahabari,

Kufuatia maagizo haya ya Mheshimiwa Rais, napenda kuwafahamisha Wananchi kuwa, kuanzia tarehe 1 Julai, 2018 Hospitali zote za Rufaa za Mikoa (Regional Refferal Hospitals) sasa zinawajibika moja kwa moja kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, Wizara inatoa shukrani za pekee kwa wadau wote ambao wamekuwa nasi bega kwa bega katika kuhakikisha utoaji wa huduma unaendelea bila kuathiriwa katika kipindi cha mpito wakati wa makabidhiano.

Jumla ya hospitali ambazo Wizara imezipokea kutoka OR-TAMISEMI ni 28, ambazo ni; Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mount Meru (Arusha), Dodoma General (Dodoma), Kitete (Tabora), Shinyanga, Geita, Singida, Mpanda (Katavi), Mawenzi (Kilimanjaro), Bombo (Tanga), Morogoro, Ligula (Mtwara), Sokoine (Lindi), Maweni (Kigoma), Sekou Toure (Mwanza), Mwananyamala, Amana, Temeke (Dar es Salaam), Songwe, Kibena (Njombe), Iringa, Tumbi (Pwani), Sumbawanga (Rukwa), Bariadi (Simiyu), Musoma (Mara), Songea (Ruvuma), Mbeya, Babati (Manyara) na Bukoba (Kagera).

Hospitali hizi zina **jumla ya vitanda 7,474** na **jumla ya watumishi 8,671** ambao, kati yao Wauguzi ni 3,960, Madaktari 536, Madaktari Bingwa wa fani mbalimbali ni 182, na waliobakia ni watumishi wa kada zingine mbalimbali za Afya. Aidha, kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2018, jumla ya wagonjwa na wateja 1,637,835 walitumia huduma katika Hospitali za Rufaa za Mikoa. Hii ni sawa na wastani wa wagonjwa 181,982 kwa mwezi.

Ndugu Wanahabari,

Wizara ya Afya inatambua na kuthamini kazi nzuri iliyofanywa katika hospitali hizi chini ya usimamizi wa OR-TAMISEMI. Vile vile itambulike kwamba Wizara imekuwa ikifanya uhakiki wa ubora wa huduma kwenye vituo vya kutolea huduma nchini, na hivi karibuni ilifanya uhakiki huo kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa na kubaini mapungufu mbalimbali yakiwemo; -

- Muundo uliopo wa uongozi na mfumo wa uendeshaji wa hospitali haukidhi mahitaji ya huduma kwa wakati wa sasa.
- Kuna upungufu wa watumishi wa 36%.
- Hali ya miundombinu na mitambo hairidhishi hususani kwa ajili ya huduma za kibingwa. Vilevile, kuna ukosefu wa baadhi ya vifaa tiba na vya uchunguzi. Aidha kasi kubwa ya mabadiliko ya teknolojia yameathiri uwezo wa hospitali hizi kumudu upatikanaji na matengenezo ya vifaa husika.
- Mifumo ya uendeshaji wa huduma na upashanaji taarifa imepitwa na wakati kulingana na mabadiliko ya teknolojia.
- Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuwezesha uendeshaji wenye tija na utoaji huduma wenye ubora katika Hospitali za Rufaa.

Ndugu Wanahabari,

Kufuatia hali hiyo, Wizara imeandaa mpango wa kuboresha huduma katika Hospitali za Rufaa za Mikoa wenye mwelekeo wa kuzipatia hospitali hizi mamlaka ya kujisimamia na kujiendesha, lakini zikiwa chini ya uangalizi wa karibu wa WAMJW, ili kuongeza kasi ya uwajibikaji na kuleta matokeo ya haraka katika kufikisha huduma bora za Rufaa kwa wananchi. Utekelezaji wa mpango huu utafanyika kwa awamu mbili;

Awamu ya kwanza; -

1. Miundombinu ya huduma itaboreshwa na kipaumbele tumeweka katika maeneo matatu (3); -
    a. Matibabu kwa wagonjwa wa dharura (Emergency Medical Services)
    b. Huduma za upasuaji wa dharura hususan wakati wa ujauzito na uzazi,
    c. Huduma za tiba kwa wagonjwa mahututi (Intensive Care Units, ICU) zikiwemo za watoto wachanga (Neonatal ICU).

    Hivyo, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara imetenga Tsh. Bilioni 30 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya kipaumbele niliyoitaja hapo juu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ambako tayari huduma zinatolewa.

    Wizara pia, imetenga jumla ya Tsh. Bilioni 10 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa miundombinu ya Hospitali za Rufaa za Mikoa katika mikoa 3 ambayo inatumia Hospitali za Wilaya kama Hospitali za Rufaa za Mikoa ambayo ni Geita, Simiyu na Njombe na kuanza ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa katika mikoa ya Songwe na Katavi.
2. Kuhakikisha uwepo wa Madaktari Bingwa, hasa katika fani 8 za kipaumbele ambazo ni; (i) Upasuaji wa jumla (General Surgery), (ii) Magonjwa ya Wanawake na Uzazi (Obstetrics & Gynaecology), (iii) Magonjwa ya Watoto (Paediatrics & Child Health), (iv) Magonjwa ya ndani (Internal Medicine), (v) Afya ya Kinywa na Meno (Dentistry), (vi) Radiolojia (Radiology), (vii) Tiba ya Usingizi (Anesthesiology) na (viii) Afya ya Macho (Opthalmology). Katika mwaka 2017/18 jumla

ya nafasi 155 zimetengwa kwa ajili ya kuajiri Madaktari ambapo, kati ya hao 41 ni Madaktari Bingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Aidha, Wizara imeidhinisha uhamisho wa Madaktari Bingwa 48 kutoka Hospitali mbalimbali nchini ambako wako wengi kwenda kufanya kazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ili, wakaimarishe huduma za matibabu ya kibingwa hasa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa zenye upungufu mkubwa. Uhamisho huu pia umehusisha Madaktari waliofuzu masomo ya kibingwa toka kituo cha awali kabla ya kuhitimu.

Vile vile, katika mwaka 2017/18, Wizara imetoa ufadhili wa masomo ya shahada ya uzamili (Masters degree) kwa Madaktari walioajiriwa katika Hospitali za umma 94 ambao baadhi yao wakihitimu watapangwa kufanya kazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Aidha, uwiano wa watumishi hasa Madaktari Bingwa utazingatiwa ili kuwa na tija zaidi katika Hospitali zote za Rufaa za Mikoa.

3. Huduma za uchunguzi wa maabara na mionzi zitaimarishwa kwa kuhakikisha kuwa kuna vifaa vya kisasa kwa ajili ya vipimo na mfumo mzuri wa matengenezo kinga ya vifaa husika. Kipaumbele kitawekwa katika upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa mionzi kwa kutumia mfumo wa digitali (digital x-rays), ultrasound.
4. Kutokana na Hospitali hizi kuhamia Wizara ya afya miundo yake ya kiungozi na uendeshaji itabadilika ili kuleta ufanisi zaidi wa kiutendaji.
5. Bodi za Ushauri wa Hospitali (Advisory Boards) zilizopo sasa zitaimarishwa ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa tija zaidi ikiwa ni hatua ya kuelekea kwenye kuzipa hadhi ya bodi tendaji.
6. Mfumo mzima wa motisha na vivutio kwa watumishi unatazamwa upya ili kuboresha na kuwavutia watumishi waliopo wadumu katika vituo husika na kuvutia wengine. Aidha, Hospitali za Rufaa za Mikoa zitaboreshwa ili kukidhi kutumika kwa ajili ya huduma za mafunzo kwa vitendo (Internship) hivyo kuchangia katika upatikanaji wa watumishi wa Afya wenye sifa.
7. Uratibu wa huduma za kibingwa kwa mkoba utaimarishwa ambapo Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kushirikiana na Hospitali za Rufaa

za Kanda na Taifa zitapeleka huduma hizo hadi ngazi ya Wilaya hasa katika maeneo yenye uhitaji mkubwa ikiwemo Upasuaji wa jumla (General Surgery), Magonjwa ya Wanawake na Uzazi (Obstetrics & Gynaecology) na Magonjwa ya Watoto (Paediatrics & Child Health).

8. Mikakati ya kuboresha huduma kwa mteja itaimarishwa ili, kufanya utoaji wa huduma kuwa rafiki zaidi na kuepuka malalamiko ya wateja yasiyo ya msingi.
9. Mfumo wa mawasiliano na upashanaji wa taarifa za hospitali na wadau wake ikiwemo jamii utaimarishwa kwa kutumia teknolojia ya kieletroniki.

Ndugu Wanahabari,

Maboresho ya Awamu ya Pili yatahusu Hospitali ya Rufaa ya Mkoa itakayokuwa imehitimu vigezo vilivyowekwa vya kuboresha huduma *(performance graduation)*. Hivyo Wizara itafanya yafuatayo; -

1. Kuanzisha Bodi ya Utendaji badala ya Bodi ya Ushauri kwa hospitali husika iliyofikia vigezo.
2. Kuboresha zaidi Muundo na mfumo wa uendeshaji wa hospitali ambapo mamlaka ya kiongozi wa hospitali itapanda na kuwa Mkurugenzi wa hospitali ambaye ataongoza wakuu wa idara.

Ndugu Wanahabari,

Wizara imeandaa utaratibu kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji mzuri wa majukumu ya uendeshaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ambapo **Hospitali itawajibika moja kwa moja kwa Wizara ya Afya kupitia kwa Katibu Mkuu - Afya kwa masuala yote ya kiutawala na kitaalam**. Menejimenti ya Hospitali itakuwa na wajibu wa kuwasilisha rasimu ya mipango ya hospitali ili kupata ushauri wa wawakilishi wa watumiaji wa huduma ndani ya Mkoa husika pamoja na kutoa mrejesho wa utekelezaji wa mipango waliyojiwekea. Aidha, Hospitali itakuwa na **wajibu wa kuwasilisha nakala ya taarifa za utekelezaji wa majukumu yake kwa Katibu Tawala wa Mkoa** ili, taarifa hii ijumuishwe kwenye Taarifa ya Afya ya Mkoa. Ni imani yangu kuwa Wakuu wa Mikoa kupita Makatibu Tawala

wa Mikoa wataendelea kufuatilia utendaji wa Hospitali za Rufaa za Mikoa katika Mikoa yao ili kuiwezesha Serikali kutekeleza vyema wajibu wake wa kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

Katika ngazi ya Taifa, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itaendelea kushirikiana na OR-TAMISEMI katika masuala yote yanayohusu utekelezaji wa huduma za afya ngazi ya mkoa na kuhakikisha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa inapata mazingira mazuri ya ushirikiano kwa ajili ya kuboresha huduma za rufaa katika mkoa husika. Hii ni kuanzia ngazi ya Zahanati, Kituo cha Afya, Hospitali ya Wilaya/Halmashauri hadi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na hatimae kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwenda Hospitali ya Rufaa ya Kanda hadi Taifa.

Ndugu Wanahabari,

Wizara inatambua kwamba, kutokana na upungufu wa watumishi katika hospitali hizi, wagonjwa na wateja wengi wanalazimika kutofuata utaratibu wa rufaa na kuamua kwenda kutibiwa katika hospitali za Kanda na Taifa. Aidha, katika kuhakikisha ubora wa huduma unaimarika ninazitaka Hospitali zote za Rufaa za Mikoa kuweka mazingira mazuri ya mawasiliano na wateja wao. Hii ni pamoja na kuweka wazi namba za simu za mawasiliano, masanduku ya maoni na vyumba vya huduma ya malalamiko ili kuwawezesha wananchi kutoa mrejesho wa huduma wanazopata, ikiwa ni pamoja na kufikisha malalamiko yao ili yaweze kutatuliwa mara moja.

Vile vile, ninazitaka Hospitali za Rufaa za Mikoa kuhakikisha kuwa huduma kwa makundi maalumu wakiwemo watoto wenye umri wa chini ya miaka 5, wajawazito, na Wazee wasio na uwezo zinatolewa kwa mujibu wa sera, miongozo na taratibu za msamaha.

Ndugu Wanahabari,

Wizara inatoa shukrani za pekee kwa wadau wote ambao wamekuwa bega kwa bega katika kuhakikisha utoaji wa huduma unaendelea bila kuathiriwa katika kipindi cha mpito wakati wa makabidhiano

Ahsanteni kwa kunisikiliza.